# SHERIA YA KUANZISHA OFISI YA MUFTI MKUU WA ZANZIBAR NA KUWEKA USIMAMIZI BORA WA SHUGHULI ZA KIISLAM ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI


1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.


### SEHEMU YA PILI
### UANZISHWAJI, UENDESHAJI WA OFISI NA HADHI YA MUFTI MKUU


3. Kuanzishwa kwa Ofisi.
4. Kazi za Ofisi.
5. Sheria zitakazofuatwa na Ofisi.
6. Uteuzi wa Mufti Mkuu.
7. Sifa za Mufti Mkuu.
8. Hadhi ya Mufti Mkuu.
9. Kazi za Mufti Mkuu.
10. Uteuzi wa Naibu Mufti Mkuu.
11. Muda wa kushikilia Ofisi na kinga.
12. Uanzishwaji wa Baraza.
13. Kusita kuwa mjumbe wa Baraza .
14. Wajibu wa Baraza.
15. Uanzishwaji wa Kamati ya Maadili.
16. Katibu Mtendaji na sifa zake.

17. Kazi na uwezo wa Katibu Mtendaji.

18. Mratibu wa Ofisi Pemba.

19. Idara, Divisheni na Vitengo.

20. Maafisa na watumishi wengine.

**SEHEMU YA TATU**
**FAT-WA**

21. Mambo ya kutolewa fat-wa.

22. Mambo yenye kujitokeza kwenye Nchi.

23. Jukumu la kuyashughulikia maswali.

24. Hadhi ya fat-wa.

**SEHEMU YA NNE**
**URATIBU NA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA KIISLAM**

25. Usuluhishi.

26. Uratibu wa tafiti.

27. Vibali vya kidini na mapendekezo ya msamaha wa kodi.

28. Kudhibiti vitabu na kazi za sanaa za Kiislam.

29. Miongozo na Mitaala.

30. Uratibu wa wanaosilimu.

31. Uratibu na usajili wa madrasa, maahad na misikiti.

32. Utambuzi wa Maahad.

33. Jumuiya za Kiislam, zisizokuwa za Kiserikali.

34. Mhadhiri wa Kiislam wa Zanzibar.

35. Mhadhiri wa Kiislamu kutoka nje ya Zanzibar.

36. Aina za ridhaa.

37. Uratibu wa shughuli mbalimbali.

38. Vikundi vya Kiislam.

39. Ruhusa ya kuanzisha sala ya kwanza ya Ijumaa.

40. Usajili wa Ulamaa.

41. Shughuli za Kiislam kitaifa.

**SEHEMU YA TANO**
**UWEZO WA OFISI**

42. Uwezo na Mamlaka ya Ofisi.

43. Mawasiliano na Ofisi nyenginezo.

44. Kujiunga na jumuiya za kikanda au Kimataifa za maendeleo ya Kiislam.

**SEHEMU YA SITA**
**MAKOSA YA ADHABU**

45. Makosa na adhabu.

46. Adhabu ya jumla.

**SEHEMU YA SABA**
**MASHARTI YA FEDHA**

47. Fedha za Ofisi.

48. Bajeti.

49. Hesabu na ukaguzi.

50. Taarifa ya Mwaka.

**SEHEMU YA NANE**
**MASHARTI MENGINEYO**

51. Kazi mtambuka.

52. Kanuni.

53. Kanuni za maadili na Miongozo.

54. Kufuta na kubakiza.

**SHERIA NAM. 4 YA 2021**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

12 Oktoba, 2021

# SHERIA YA KUANZISHA OFISI YA MUFTI MKUU WA ZANZIBAR NA KUWEKA USIMAMIZI BORA WA SHUGHULI ZA KIISLAM ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar, 2021 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Ofisi" maana yake ni Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar kama ilivyoanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"Baraza" maana yake ni Baraza la Ulamaa lililoanzishwa chini ya kifungu cha 12 cha Sheria hii;

"Fat-wa" maana yake ni ufumbuzi wa mwisho unaotolewa na Mufti Mkuu kwa maslahi ya umma juu ya jambo lolote la Kiislam lenye utata au kukinzana linalowasilishwa kwake kulitolea maamuzi au vyenginevyo;

"Kamati" maana yake ni Kamati ya Maadili iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 15 cha Sheria hii;

"Katibu Mtendaji" maana yake ni Katibu Mtendaji wa Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 16 cha Sheria hii;

"Mufti Mkuu" maana yake ni mtu anayeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 6 cha Sheria hii;

"Mhadhara" maana yake ni mkusanyiko wa watu kwa madhumuni ya kusikiliza au kujadili jambo la Kiislam;

"Mhadhiri" maana yake ni mzungumzaji au muwasilishaji mkuu katika mkusanyiko wa watu kwa madhumuni ya kuwasilisha mada au kujadili jambo la Kiislamu;

"Maahad" maana yake ni chuo kinachotoa elimu ya Kiislam kwa mfumo rasmi kuanzia ngazi ya msingi, sekondari hadi stashahada;

"Naibu Mufti Mkuu" maana yake ni mtu anayeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 10 cha Sheria hii;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Vikundi vya Kiislam" maana yake ni vikundi vya Kiislam visivyosajiliwa kama Jumuiya ya Kiislam na inajumuisha kila kikundi cha dhikri, ruq-ya, dufu na mfano wa hivyo;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na mambo yanayohusiana na masuala ya Ofisi ya Mufti Mkuu;

"Shura" maana yake ni kikao au mkutano wa Ulamaa kujadili jambo lolote linalohusu masuala ya dini ya Kiislam;

"Ulamaa" maana yake ni mwanachuoni wa Kiislam mwenye elimu ya kutosha ya fani mbali mbali za dini ya Kiislam na lugha ya kiarabu.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHWAJI, UENDESHAJI NA HADHI YA OFISI YA MUFTI MKUU

Kuanzishwa kwa Ofisi.

**3.**-(1) Kunaanzishwa Ofisi itakayojulikana kama Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar.

(2) Ofisi itakuwa ni Ofisi inayojitegemea na yenye muhuri rasmi.

(3) Muhuri rasmi wa Ofisi utatumika kwa namna itakavyoelekezwa na Mufti Mkuu.

(4) Ofisi inaweza kuanzisha ofisi ndogo katika Wilaya itakapojitokeza haja ya kufanya hivyo.

Kazi za Ofisi.

**4.**-(1) Ofisi itakuwa na kazi za:

(a) kufanya utafiti kuhusiana na masuala ya Kiislam;

(b) kupokea masuala yote yanayohitaji kupatiwa fat-wa, majibu au maelekezo kwa mujibu wa Sheria hii;

(c) kutoa miongozo ya dini ya Kiislam kwa maslahi ya umma;

(d) kuratibu na kusimamia uandaaji wa mihadhara, warsha, semina na shughuli nyengine za Kiislam;

(e) kuratibu kazi za kitafiti za Kiislam zinazoandaliwa na taasisi za Serikali au taasisi binafsi au mtu yeyote;

(f) kuratibu, kusajili na kuweka kumbukumbu na taratibu za uendeshaji wa ulamaa, misikiti, madrasa, maahad, taasisi, makundi na jumuiya za Kiislam;

(g) kupendekeza usajili wa jumuiya za Kiislam kwa mujibu wa sheria inayosimamia Jumuiya zisizo za kiserikali;

(h) kuwaidhinisha wahadhiri wa Kiislam kutoka nje ya Zanzibar baada ya kuridhishwa na malengo na uwezo wao pamoja na maadili;

(i) kudhibiti na kuidhinisha uingizwaji, usambazaji wa vitabu vya Kiislam na tafsiri ya vitabu vya Kiislam kwa njia yoyote;

(j) kuratibu sherehe au maadhimisho ya Kiislam na kutangaza kuandama kwa mwezi kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Ofisi inaweza kuyatekeleza, kuyaratibu au kuyasimamia mambo yote iliyopewa Mamlaka kwa mujibu wa Sheria hii.

Sheria zitakazofuatwa na Ofisi.

**5.** Ofisi itatekeleza, itaratibu na itasimamia kazi zake kwa kufuata Sheria za Kiislam, Sheria hii, sheria nyengine na Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

Uteuzi wa Mufti Mkuu.

**6.**-(1) Kutakuwa na Mufti Mkuu wa Zanzibar ambaye atateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Baraza.

(2) Mufti Mkuu atalipwa mshahara na maslahi mengine kama itakavyoidhinishwa na Rais.

Sifa za Mufti Mkuu.

**7.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mufti Mkuu ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari, mwanamme, muislamu mwenye uadilifu na mwenye umri usiopungua miaka arubaini;

(b) anayo elimu ya kutosha ikiwemo Qur-ani, Sunna na fiqhi;

(c) anaheshimika na kukubalika mbele ya wanachuoni na jamii ya Kiislam kwa ujumla;

(d) hafungamani na upande wowote wa kisiasa.

Hadhi ya Mufti Mkuu.

**8.** Mufti Mkuu atakuwa:

(a) ndiye Kiongozi Mkuu wa Waislamu wote kwa Zanzibar na atakuwa na jukumu la kutoa "fat-wa", kutekeleza na kusimamia shughuli nyenginezo za Waislamu; na

(b) kwa hadhi yake au mtu mwengine atakayemuidhinisha kwa niaba yake, atakuwa Msemaji Mkuu na Mwakilishi wa Waislamu wote wa Zanzibar kwa mambo yote ya Kiislam ndani na nje ya nchi.

Kazi za Mufti Mkuu.

**9.**-(1) Mufti Mkuu atakuwa na kazi za:

(a) kutoa "fat-wa" juu ya jambo lolote kwa mujibu wa mtazamo wa Kiislam;

(b) kutoa maamuzi na miongozo ya Kiislam kwa mujibu wa Sheria hii; na

(c) kutangaza kuandama kwa mwezi.

(2) Mufti Mkuu atatekeleza majukumu yake chini ya kifungu hiki kwa kushauriana na Baraza.

(3) Bila ya kuathiri masharti yoyote ya Sheria hii, Mufti Mkuu akiwa hayupo au kwa sababu nyengine yoyote anashindwa kutekeleza kazi zake, Naibu Mufti Mkuu atafanya kazi na kutumia uwezo wa Mufti Mkuu.

Uteuzi wa Naibu Mufti Mkuu.

**10.**-(1) Kutakuwa na Naibu Mufti Mkuu wa Zanzibar atakayeteuliwa na Rais.

(2) Sifa na masharti ya uteuzi wa Mufti Mkuu yatatumika katika uteuzi wa Naibu Mufti Mkuu.

(3) Naibu Mufti Mkuu atakuwa ndiye Msaidizi Mkuu wa Mufti Mkuu.

Muda wa kushikilia Ofisi na kinga.

**11.**-(1) Mufti Mkuu au Naibu Mufti Mkuu atashika madaraka yake mpaka pale ambapo:

(a) uteuzi wake utakapofutwa na Rais;

(b) atakapofariki dunia; au

(c) atakapojiuzulu.

(2) Rais, katika kutumia uwezo wake chini ya kifungu kidogo cha (1) (a) cha kifungu hiki, atazingatia mapendekezo ya Kamati ya Uchunguzi atakayoiunda kwa ajili ya kuchunguza na kubainisha sababu za kumuondoa au kutokumuondoa katika madaraka Mufti Mkuu au Naibu Mufti Mkuu.

(3) Rais, katika kuanzisha Kamati ya Uchunguzi iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, atazingatia Wanachuoni wa Kiislam.

Uanzishwaji wa Baraza.

**12.**-(1) Kunaanzishwa chombo cha kumshauri Mufti Mkuu kitakachojulikana kama Baraza la Ulamaa la Zanzibar.

(2) Baraza litaundwa na:

(a) Mufti Mkuu ambaye atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Baraza;

(b) Kadhi Mkuu;

(c) Naibu Mufti Mkuu;

(d) Naibu Kadhi Mkuu;

(e) Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana;

(f) Sheikh mmoja kutoka kila Wilaya; na

(g) Wajumbe wengine wawili kwa kuzingatia madhehebu yao ya dini ya Kiislam.

(3) Wajumbe waliotajwa chini ya aya ya (f) na (g) ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, watateuliwa na Mufti Mkuu kulingana na uzoefu, elimu na taaluma inayohusiana na mambo ya Kiislam.

(4) Katibu Mtendaji atakuwa Katibu wa Baraza.

(5) Utaratibu wa mikutano, muda wa wajumbe na mambo mengine ya uendeshaji wa mikutano ya Baraza yatakuwa kama yatakavyoainishwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(6) Mufti Mkuu anaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria kwenye kikao chochote kwa madhumuni ya kutoa mapendekezo yake kuhusu jambo linalojadiliwa.

Kusita kuwa mjumbe wa Baraza.

**13.** Mjumbe yeyote aliyetajwa kwenye kifungu cha 12 kifungu kidogo cha (2) aya ya (f) na (g) atasita kuwa mjumbe wa Baraza ikiwa:

(a) atafariki dunia;

(b) atajiuzulu;

(c) atashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo; au

(d) ataondolewa na Mufti Mkuu kutokana na tabia mbaya au kukosa sifa zilizomuwesha kuteuliwa kuwa mjumbe.

Wajibu wa Baraza.

**14.**-(1) Baraza litamshauri Mufti Mkuu juu ya masuala ya Kiislam yatakayowasilishwa kwake kwa madhumuni ya kutolewa "fat-wa" na litafanya kazi nyengine yoyote kama itakavyoamuliwa na Mufti Mkuu.

(2) Maamuzi ya Mufti Mkuu baada ya kupata ushauri wa Baraza katika kutowa "fat-wa" yatakuwa ndiyo maamuzi ya mwisho.

Uanzishwaji wa Kamati ya Maadili.

**15.**-(1) Kunaanzishwa Kamati ya Maadili katika Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na Mwenyekiti wake atakuwa Katibu Mtendaji.

(2) Mufti Mkuu atateua wajumbe watatu (3) wa Kamati ya Maadili ambao hawatokani miongoni mwa wajumbe wa Baraza.

(3) Kazi, sifa za wajumbe wa Kamati ya Maadili na utaratibu wa mkutano utakuwa kama itakavyoainisha katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Katibu Mtendaji na sifa zake.

**16.**-(1) Kutakuwa na Katibu Mtendaji wa Ofisi ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Katibu Mtendaji ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) Muislamu;

(c) anayo angalau shahada ya kwanza katika masuala ya Kiislam;

(d) ana uzoefu wa kazi angalau miaka minne (4) katika masuala ya utawala wa umma; na

(e) ni muadilifu.

Kazi na uwezo wa Katibu Mtendaji.

**17.** -(1) Katibu Mtendaji atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu na Afisa Masuul wa Ofisi.

(2) Katibu Mtendaji atawajibika kusimamia na kutekeleza kazi za kila siku za Ofisi ikiwa ni pamoja na:

(a) kusimamia watumishi, mambo ya kifedha na shughuli nyenginezo;

(b) kuandaa mipango ya kazi, bajeti na mambo mengine ya kiutawala;

(c) kuratibu shura zote za Baraza;

(d) kutunza na kuweka kumbukumbu za "fat-wa" zote zinazotolewa na Mufti Mkuu;

(e) kusajili fat-wa zote zinazotolewa na Mufti Mkuu;

(f) kuchapisha "fat-wa" zote katika Gazeti Rasmi la Serikali;

(g) kuandaa ripoti mbali mbali kama zitakavyohitajika kwa mujibu wa sheria zilizopo; na

(h) kufanya kazi nyengine yoyote ya Ofisi kwa mujibu wa Sheria hii.

Mratibu wa Ofisi Pemba.

**18.**-(1) Kutakuwa na Mratibu wa Ofisi Pemba ambaye atateuliwa na Mufti Mkuu.

(2) Mratibu aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atakuwa ni Msaidizi Mkuu wa Katibu Mtendaji kwa Pemba na katika utekelezaji wa kazi za Ofisi atawajibika kwa Katibu Mtendaji.

Idara, Divisheni na Vitengo.

**19.** Ofisi inaweza kuanzisha Idara, Divisheni na Vitengo kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

Maafisa na watumishi wengine.

**20.** Ofisi inaweza kuajiri maofisa na watumishi wengine kama itakavyohitajika kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma kwa madhumuni ya utekelezaji wa kazi za Ofisi.

## SEHEMU YA TATU
## "FAT-WA"

Mambo ya kutolewa "fat-wa".

**21.** Mufti Mkuu atakuwa na jukumu la kutoa "fat-wa" au majibu kwa kutafsiri masharti ya hukmu za Kiislam kwa mujibu wa mijadala ya sheria za Kiislam kwenye mambo yanayojumuisha itikadi, ibada, miamala, ndoa, talaka, mirathi, wakfu, amana, wasia, hiba na mfano wa hayo yatakayowasilishwa au kuulizwa na taasisi au mtu yeyote.

Mambo yenye kujitokeza kwenye Nchi.

**22.** Mufti Mkuu atakuwa na jukumu la kutoa "fat-wa" juu ya jambo lolote la dharura au lililojitokeza na kuwasilishwa kwake kwa utaratibu wowote, linalohusu swali lolote la Kiislam au jambo lililojitokeza nchini, kwenye jamii au jambo jengine ambalo linahitaji kuamuliwa.

Jukumu la kuyashughu-likia maswali.

**23.** Ofisi itakuwa na jukumu la kutoa elimu kwa watu na kuwapa "fat-wa" au majibu kwa wanaohitaji ufafanuzi wa masharti ya hukmu za Kiislam.

Hadhi ya "fat-wa".

**24.**-(1) "Fat-wa" yoyote itakayotolewa na Mufti Mkuu juu ya jambo lolote itakuwa ndiyo msimamo wa kisheria na "fat-wa" hiyo itatumika Zanzibar kwa jambo hilo.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, "fat-wa" itakayopata hadhi hiyo itatamkwa na Mufti Mkuu na hatimaye kuandikwa kwa maandishi na kusainiwa na yeye mwenyewe.

(3) Ofisi itaziweka kwenye kumbukumbu, kuzisajili na kuzichapisha "fat-wa" zote katika Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na kuzitolea taarifa kupitia vyombo vya habari vya umma.

## SEHEMU YA NNE
## URATIBU NA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA KIISLAM

Usuluhishi.

**25.**-(1) Ofisi itakuwa na wajibu wa kusuluhisha mgogoro wowote utakaotokezea baina ya:

(a) Waislamu kwa Waislamu;

(b) Waislamu na wasiokuwa Waislamu;

(c) Vikundi vya dini na taasisi mbali mbali.

(2) Katika kusuluhisha mgogoro uliotajwa katika kifungu kidogo cha (1) aya (b) na (c) ya kifungu hiki, Ofisi inaweza kushirikiana na viongozi wa dini hizo nyengine na taasisi mbali mbali.

(3) Ofisi inaweza kuweka utaratibu wa jinsi ya kuwasilisha mgogoro wowote unaohitaji kusuluhishwa chini ya Sheria hii.

Uratibu wa tafiti.

**26.** Ofisi itafanya, itaratibu au itashirikiana na taasisi za umma au binafsi au mtu yeyote katika ufanyaji wa tafiti Zanzibar juu ya jambo lolote la Kiislam.

Vibali vya kidini na mapendekezo ya msamaha wa kodi.

**27.** Ofisi inaweza kutoa vibali na mapendekezo katika masuala yanayohusu dini ya Kiislam ikiwemo:

(a) vibali katika kuchangisha fedha kwa ajili ya msaada wa matibabu, ujenzi, ukarabati wa misikiti, madrasa, maahad na mfano wa hayo.

(b) kutoa mapendekezo kwa mamlaka zinazohusika, kwa msamaha wa kodi kwa uingizaji wowote wa vifaa au vitu vyengine vitakavyotumika kwa shughuli za kidini Zanzibar.

Kudhibiti vitabu na kazi za sanaa za Kiislam.

**28.** Ofisi itakuwa na wajibu wa kudhibiti na kuidhinisha uingizaji, usambazaji, tafsiri na matumizi ya vitabu vyote vya Kiislam pamoja na kazi za sanaa za Kiislam.

Miongozo na Mitaala.

**29.**-(1) Ofisi itashirikiana na Wizara inayohusika na elimu katika kuandaa na kukuza miongozo na mitaala ya elimu ya dini ya Kiislam kwa skuli na vyuo vya Zanzibar.

(2) Ofisi inaweza, kwa kushirikiana na Wizara inayohusika na elimu, kuweka miongozo ya ufundishaji kwa madrasa na maahad za Zanzibar.

Uratibu wa wanaosilimu.

**30.** Ofisi itaweka utaratibu wa kutoa vyeti vya uthibitisho kwa kila mtu anayeingia kwenye dini ya Kiislam kwa njia ya kusilimu.

Uratibu na usajili wa madrasa, maahad na misikiti.

**31.**-(1) Ofisi itasajili madrasa, maahad na misikiti yote ya Zanzibar.

(2) Ofisi itaratibu na kusimamia shughuli za madrasa, maahad na misikiti yote ya Zanzibar na kutoa maelekezo.

(3) Ofisi inaweza kufuta usajili wa madrasa, maahad au msikiti wowote chini ya kifungu hiki, iwapo uongozi wake utashindwa kufuata Sheria hii, Kanuni, au miongozo, maelekezo yaliyotolewa.

(4) Mtu yeyote ambaye hajaridhika na maamuzi yaliyotolewa chini ya kifungu hiki, anaweza kukata rufaa kwa Waziri.

(5) Waziri anaweza kutunga Kanuni kuhusiana na taratibu za kukata rufaa chini ya kifungu hiki.

Utambuzi wa Maahad.

**32.**-(1) Ofisi itakuwa na uwezo wa kuziainisha, kuzithibitisha na kuzipatia vyeti vya usajili maahad zote za Zanzibar pamoja na ngazi zake za kielimu.

(2) Ofisi, kwa kushirikiana na Wizara inayohusika na elimu, itahakikisha inasaidia kutambulika rasmi kwa maahad na ngazi zake za kielimu ndani ya Tanzania.

Jumuiya za Kiislam zisizokuwa za kiserikali.

**33.**-(1) Bila ya kujali masharti mengineyo chini ya sheria inayosimamia Jumuiya zisizo za Kiserikali, Jumuiya yoyote ya Kiislam isiyokuwa ya kiserikali haitasajiliwa Zanzibar kabla ya kupatikana kwanza mapendekezo ya maandishi kutoka katika Ofisi.

(2) Masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki yatazihusu Jumuiya za Kiislam zisizokuwa za kiserikali za ndani ya nchi, kikanda na kimataifa.

Mhadhiri wa Kiislam wa Zanzibar.

**34.**-(1) Mhadhiri wa Kiislam wa Zanzibar hatofanya mhadhara nje ya msikiti bila ya kupata ridhaa ya maandishi kutoka katika Ofisi.

(2) Ofisi inaweza kutoa ridhaa ya maandishi kwa mhadhiri yeyote wa dini ya Kiislam wa ndani ya Zanzibar baada ya kuridhika na uwezo na maadili yake.

Mhadhiri wa Kiislam kutoka nje ya Zanzibar.

**35.**-(1) Mhadhiri yeyote wa dini ya Kiislam kutoka nje ya Zanzibar hatofanya mhadhara bila ya kupata ridhaa ya maandishi kutoka katika Ofisi.

(2) Ofisi inaweza kutoa ridhaa ya maandishi kwa mhadhiri yeyote wa dini ya Kiislam kutoka nje ya Zanzibar baada ya kuridhika na uwezo na maadili yake.

(3) Mhadhara uliotajwa katika kifungu hiki unajumuisha mawaidha ya ndani au nje ya msikiti, kwenye redio au televisheni.

Aina za ridhaa.

**36.**-(1) Ofisi inaweza kutoa ridhaa ya maandishi ya kudumu au ya muda kwa mhadhiri yeyote wa dini ya Kiislam wa ndani ya Zanzibar baada ya kuridhika na uwezo wake na maadili yake.

(2) Hakutakuwa na ridhaa ya kudumu itakayotolewa kwa namna yoyote kwa Mhadhiri wa dini ya Kiislam kutoka nje ya Zanzibar.

Uratibu wa shughuli mbali mbali.

**37.**-(1) Ofisi itaratibu na kusimamia matayarisho ya mihadhara, warsha, semina, makongamano na shughuli nyenginezo za Kiislam hapa Zanzibar.

(2) Mtu yeyote hatofanya jambo lolote lililotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, bila kupeleka taarifa katika Ofisi na kukubaliwa kwa maandishi.

Vikundi vya Kiislam.

**38.**-(1) Ofisi inaweza kuratibu na kusimamia vikundi vya Kiislam Zanzibar na kutoa miongozo pale inapohitajika kufanya hivyo.

(2) Ofisi itasajili na ıtatunza kumbukumbu za vikundi vyote vya Kiislam Zanzibar.

Ruhusa ya kuanzisha sala ya kwanza ya Ijumaa.

**39.** Ofisi itakuwa na mamlaka ya pekee ya kutoa ruhusa ya kuanza kwa mara ya kwanza kusaliwa sala za Ijumaa ya kwanza kwa misikiti ya Zanzibar.

Usajili wa Ulamaa.

**40.** (1) Ofisi itasajili na itatunza kumbukumbu za Ulamaa wote wa Zanzibar.

(2) Ofisi itaweka utaratibu wa usajili wa Ulamaa Zanzibar.

Shughuli za Kiislam kitaifa.

**41.**-(1) Ofisi itaratibu shughuli za Kiislam zifuatazo:

(a) Sala ya Iddi ya kitaifa na Baraza la Iddi kitaifa;

(b) Maulidi ya Siku ya Kuzaliwa Mtume Muhammad (SAW) kitaifa; na

(c) Shughuli nyengine yoyote ya Kiislam ambayo Serikali itaamua iratibiwe kitaifa na Ofisi.

(2) Ofisi inaweza kuunda Kamati kufanikisha shughuli zote zilizotajwa chini ya kifungu hiki.

(3) Shughuli zote za Kiislam kitaifa hapa Zanzibar zitathibitishwa na Ofisi pekee.

## SEHEMU YA TANO
## UWEZO WA OFISI

Uwezo na Mamlaka ya Ofisi.

**42.** Ofisi, kwa madhumuni ya kufanikisha utekelezaji wa kazi zake, inaweza:

(a) kumuita mtu yeyote au kikundi cha watu au taasisi yoyote kwa madhumuni ya kutatua mgogoro wowote wa kidini au jambo lolote lililo katika mamlaka yake;

(b) kutoa amri, katazo, maelekezo au kuweka masharti yoyote kuhusu jambo lolote linalohusu mamlaka yake;

(c) kutoa au kufuta ruhusa ya kudumu au ya muda kuhusu harakati zozote za Kiislam ikijumuisha ijitimai, mihadhara au mikusanyiko mengine ya Kiislam ndani ya Zanzibar;

(d) kumkataza au kumzuia mhadhiri wa Kiislam wa ndani au wa nje ya Zanzibar kufanya mhadhara baada ya kujiridhisha kwamba mhadhiri huyo hana sifa za Kiislam, amekosa uwezo au hana maadili katika uislamu au anahatarisha amani na utulivu;

(e) kumkataza au kumzuia mwalimu yeyote wa madrasa wa ndani au wa nje ya Zanzibar kufanya kazi ya kusomesha au kushiriki shughuli yoyote ndani ya madrasa au maahad hiyo baada ya kujiridhisha kuwa mwalimu huyo:

(i) hana tabia njema;

(ii) anavunja maadili ya Kiislam;

(iii) anashutumiwa kwa udhalilishaji wa watoto au wanawake;

(iv) hana sifa au uwezo katika masuala ya dini ya Kiislam; au

(v) anahatarisha amani na utulivu;

(f) kufunga au kubadilisha kwa muda, matumizi ya jengo la msikiti, madrasa au maahad pindi pakitokezea uvunjifu wa amani au uvunjifu wa maadili ya Kiislam; na

(g) kutoa kauli au kukemea juu ya jambo lolote lililogusa hisia za Waislamu.

Mawasiliano na Ofisi nyengine zinazofanana na hizo.

**43.** Ofisi inaweza kuwasiliana na Ofisi nyengine za mfano wake hapa Nchini, Kikanda na Kimataifa kwa lengo la kujenga uhusiano, kubadilishana uzoefu, taaluma na fikra mpya zinazohusiana na mambo mbali mbali ya Kiislam.

Kujiunga na jumuiya za kikanda au kimataifa za maendeleo ya Kiislam.

**44.** Kwa idhini ya Waziri, Ofisi inaweza kujiunga katika jumuiya yoyote ya Kiislam ya Kikanda au ya Kimataifa ambayo inashughulikia maendeleo ya Kiislam.

## SEHEMU YA SITA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu.

**45.** Mtu yeyote ambaye:

(a) ataingilia majukumu ya Ofisi yaliyoelezwa chini ya Sheria hii;

(b) atadharau au atakataa wito wa Ofisi bila ya sababu za msingi;

(c) atadharau au atashindwa kutii amri, katazo, maelekezo au masharti yaliyotolewa chini ya Sheria hii; au

(d) atafanya harakati zozote za Kiislam nje ya msikiti ikijumuisha ijitimai, mihadhara au mikusanyiko mengine ya Kiislam ndani ya Zanzibar bila ya ruhusa ya Ofisi,

ametenda kosa na akipatikana na hatia:

(i) atafutiwa leseni au kibali alichopewa; au

(ii) atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tatu za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Moja za Kitanzania au atatumikia kifungo kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi mwaka mmoja au vyote viwili faini na kifungo.

Adhabu ya jumla.

**46.** Mtu yeyote ambaye atavunja masharti yoyote yaliyoelezwa chini ya Sheria hii au ametenda kosa ambalo hakuna adhabu chini ya Sheria hii; akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tatu za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Moja za Kitanzania au kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita au vyote viwili faini na kifungo.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha za Ofisi.

**47.** Fedha na rasilimali nyengine za Ofisi zitajumuisha:

(a) fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni ya Ofisi;

(b) mikopo au misaada inayopokelewa na Ofisi kwa ajili ya kazi zake; na

(c) fedha nyengine zozote zinazoweza kupatikana kihalali katika Ofisi.

Bajeti.

**48.**-(1) Ofisi, si chini ya miezi miwili kabla ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, itaandaa na itawasilisha kwa Waziri bajeti ya mwaka kwa ajili ya kuidhinishwa inayoonesha makadirio ya mapato yake na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Ofisi inaweza, wakati wowote kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha, kuandaa na kuwasilisha kwa Waziri kwa ajili ya kuidhinishwa makadirio yoyote ya bajeti ya ziada kwa bajeti ya mwaka wa fedha husika.

Hesabu na ukaguzi.

**49.**-(1) Ofisi itaweka hesabu na kumbukumbu za miamala yote na itahakikisha kwamba fedha zote zilizopokelewa au kulipwa na Ofisi zimetumika ipasavyo.

(2) Taarifa za fedha za mwaka za Ofisi zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Taarifa ya mwaka.

**50.**-(1) Ofisi, ndani ya miezi saba baada ya mwisho wa mwaka wa fedha, itaandaa au itawezesha kuandaliwa na itawasilisha kwa Waziri Taarifa ya Mwaka.

(2) Taarifa ya Mwaka chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa taarifa ya kina inayozingatia kazi za Ofisi katika mwaka huo wa fedha ambao unahusika, na itajumuisha:

(a) nakala ya taarifa za hesabu zilizokaguliwa za Ofisi pamoja na taarifa ya mkaguzi;

(b) taarifa ya utekelezaji ya Ofisi ya mwaka huo wa fedha; na

(c) taarifa nyengine muhimu za Ofisi kama zinavyohitajika na Sheria hii.

(3) Kwa upatikanaji wa taarifa kwa umma, baada ya idhini ya Waziri, taarifa ya mwaka ya Ofisi itachapishwa.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

Kazi mtambuka.

**51.** Bila ya kuathiri kazi na majukumu yaliyotajwa ndani ya Sheria hii au sheria nyengine zilizopo, Ofisi inaweza kufanya mambo mengine yoyote ambayo ni muafaka na ni mazuri katika kufikia malengo ya Sheria hii.

Kanuni.

**52.**-(1) Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga Kanuni kuhusiana na:

(a) taratibu za uendeshaji wa vikao vya Baraza,

(b) taratibu za uratibu wa sherehe au maadhimisho ya Kiislam;

(c) Kanuni nyengine zozote zitakazosaidia usimamizi bora wa Sheria hii.

(3) Kanuni na miongozo chini ya Sheria hii itatangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Kanuni za maadili na miongozo.

**53.**-(1) Mufti Mkuu anaweza kutunga Kanuni za Maadili na kuweka miongozo kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla chini kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mufti Mkuu anaweza kuweka miongozo mahsusi kuhusiana na namna na taratibu za:

(a) kufuatwa kabla na baada ya kutolewa fat-wa au majibu na ufafanuzi juu ya mambo ya Kiislam;

(b) utambuzi na vigezo vinavyotumika kuwatambua Ulamaa wa Zanzibar;

(c) kutangaza mwezi mwandamo;

(d) usuluhishi, utoaji wa miongozo ya Kiislam na namna ya kujenga mahusiano mema ya kijamii;

(e) uratibu, usajili na usimamizi wa shughuli za uendeshaji wa misikiti, madrasa, maahad, taasisi, jumuiya na makundi ya Kiislam yaliyotajwa chini ya Sheria hii; na

(f) miongozo mengine yoyote itakayosaidia ufanisi katika utekelezaji wa Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

**54.**-(1) Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mufti Nam. 9 ya Mwaka 2001 inafutwa.

(2) Bila ya kujali ufutwaji chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mambo yote yaliyofanywa chini ya Sheria iliyofutwa yatahesabika kuwa yamefanywa chini ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 9 Septemba, 2021.

.............................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***